mkongetv | @bodiyamkongetz

# JARIDA LA MKONGE

ISSUE NO. 06 | 31 DESEMBA 2024

MKONGE NI BIASHARA, WEKEZA SASA



## WAZIRI BASHE AZINDUA KITUO ATAMIZI CHA MKONGE

# JITIHADA ZA RAIS SAMIA ZILIVYOPAISHA SEKTA YA MKONGE

## TSB KUSHIRIKIANA NA ZANZIBAR KUKUZA UTALII KUPITIA MKONGE

# BODI YA WAKURUGENZI TSB



Theobald Maingu Sabi
**MWENYEKITI**



Prof. Esther William Dungumaro
**MJUMBE**



Beatrice Agnes Singano
**MJUMBE**



Shedrack Mokiwa Lugendo
**MJUMBE**



Mohamed Hamis Chikawe
**MJUMBE**



Andrew Wilson Nkuzi
**MJUMBE**



Dk. Catherine Justin Senkoro
**MJUMBE**



Evelyne Baruti Mugasha
**MJUMBE**



Naweed Yakub Mulla
**MJUMBE**


**SAFU YA UHARIRI**
**MHARIRI MKUU**
Saddy Kambona
Mkurugenzi Mkuu

**MHARIRI**
Esther Mbusi
Afisa Uhusiano na Mawasiliano

**WAANDISHI**
Shani Chogero
Raya Kipingu

**WAPIGA PICHA**
Kelvin Beda
Juma Mngano

**MSANIFU KURASA**
Robert Julius




Mawasiliano:
Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB)
Independence Avenue/Usagara Street Mkonge House
+ 255 272 645 060
dg@sisalboard.go.tz

Jarida hili limetolewa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB)

# Tahariri ya *Mkurugenzi*

## 2024 ULIKUWA MWAKA WA MAFANIKIO, 2025 TUNATEGEMEA MAFANIKO ZAIDI

Mpendwa mdau wa Mkonge na msomaji wetu,
nakusalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Tunapokaribia kuumaliza mwaka 2024 na kuukaribisha Mwaka mpya 2025, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru nyote kwa ushirikiano wenu wa dhati. Kwa pamoja tumefanikiwa kutekeleza malengo mengi yanayohusiana na sekta ya mkonge, na mafanikio haya yametokana na juhudi zetu za pamoja.

Kipekee tunamshukuru sana Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada na juhudi alizoonyesha ambazo zimechangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa Sekta ya Mkonge katika Nyanja tofauti ikiwamo ongezeko la ajira, wakulima, wafanyabiashara na mabo kadha wa kadha.

Aidha, tunamshukuru Hussein M. Bashe, Waziri wa Kilimo, kwa uongozi wake wa pekee na msaada wake usio na kifani katika kuendeleza sekta ya mkonge.

Katika mwaka huu, tumefanikiwa kuongeza uzalishaji wa mkonge kutoka Tani 49,752.88 hadi Tani 59,416.28 kwa mwaka na kuongeza thamani ya mauzo ya nje kutoka USD 2,624,204.52 hadi USD 4,105,561.22 kwa mwaka.

Huu ni mwaka ambao tumefanikiwa kwa pamoja katika kufikia malengo mengi. Hata hivyo, tunatambua kuwa bado tunakabiliana na changamoto kubwa ya kukosekana kwa mitambo ya kutosha ya kuchakata mkonge (makorona).

Hadi sasa, tumeweza kununua korona moja na tunaanzisha kituo cha kuchakata mkonge kwa wakulima wadogo katika kijiji cha Taula, wilayani Handeni. Vituo vingine kama hivyo vitajengwa katika maeneo ya Korogwe, Mkinga, Lushoto, Kilosa na wilaya nyingine katika mkoa wa Pwani, Manyara, Shinyanga na Singida.

Katika mwaka huu pia, tumepata gari moja la kuchimba visima vya maji ili kushughulikia tatizo la upungufu wa maji katika sekta ya mkonge na pia kusaidia sekta nyingine za kilimo. Tumeanzisha kituo cha Mkonge BBT chenye lengo la kuwajengea uwezo wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kupata maarifa kuhusu kuongeza thamani ya mazao ya mkonge kupitia ufundi wa mikono (handcraft).

Mpango wetu wa mwaka 2025 ni kuongeza uzalishaji na tija ya mkonge, kuongeza thamani ya mauzo, kuongeza matumizi ya ndani ya mkonge na bidhaa zake, kuvutia wawekezaji zaidi katika minyororo ya thamani ya mkonge, na pia kuingia katika biashara ya Hati za Kijamii za Vitendo vya Mabadiliko ya Tabianchi maarufu kama biashara ya hewa ukaa/kaboni- Climate Change Digital Receipt(CADR).

Tunawashukuru nyote kwa msaada na ushirikiano wenu. Kwa pamoja, tunaweza kuendelea kuleta maendeleo na kuboresha sekta ya mkonge nchini Tanzania.

Nawatakia heri ya Mwaka Mpya 2025!
Asanteni sana.
Saddy H. Kambona,
Mkurugenzi Mkuu,
Bodi ya Mkonge Tanzania.





# JITIHADA ZA RAIS SAMIA ZILIVYOPAISHA SEKTA YA MKONGE

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Saddy Kambona amesema katika kpindi cha Awamu ya Sita kuanzia 2021 hadi mwaka huu ndicho kipindi ambacho Bodi hiyo imefanikiwa kufanya miradi ya maendeleo zaidi kuliko wakati wowote kutokana na uwezeshwaji mkubwa uliofanywa na serikali.

Amesema ni katika kipindi hicho cha miaka mitatu bodi hiyo imepata fedha nyingi kwa ajili ya kununua mitambo ya kuchakata mkonge (korona)kwani imefamnikiwa kuhamasisha watu wengi kulima mkonge na sasa wanajitokeza wengi changamoto ilikuwa umefika wakati wa kuvuna wakulima waliopanda mwaka 2021 mwaka huu wanavuna changamoto inakuja kwenye uchache wa mashine ya kuchakata mkonge wao (korona).

"Rais Samia ametuchangia fedha kuanzia mwaka jana na mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kununua korona kutatua changamoto za wakulima wadogo ambapo kuna nne ziko njiani ambazo zitafungwa katika wilaya za Mkinga. Lushoto na Kilosa. Moja tayari imeshafika kwenye hatua za mwisho za kusimikwa huko Taula wilayani Handeni.

"Ametoa fedha kwa ajili ya kuhamasisha zao kwa kusambaza mbegu za Mkonge bure takribani Sh milioni 500 na bodi imesambaza mbegu hizo takribani nchi nzima kwa wakulima," alisema Mkurugenzi Kambona.

"Lakini pia ni kipindi ambacho bodi haikuwa na jengo lake la ofisi lakini ndani ya muda mfupi alitupatia fedha kukarabati ofisi hiyo, alitubadilishia muundo wetu wa ofisi, tukafungua ofisi za kanda lakini pia tumefanikiwa watumishi wa kutosha ongezeko la watumishi kutoka 32 hadi 56 waliopo kazini sasa," alisema Mkurugenzi Kambona.

"

*Lakini pia ni kipindi ambacho bodi haikuwa na jengo lake la ofisi lakini ndani ya muda mfupi alitupatia fedha kukarabati ofisi hiyo, alitubadilishia muundo wetu wa ofisi, tukafungua ofisi za kanda lakini pia tumefanikiwa watumishi wa kutosha ongezeko la watumishi kutoka 32 hadi 56 waliopo kazini sasa," alisema Mkurugenzi Kambona.*

Alisema jitihada hizo zote ni kwa sababu Rais Samia ameona kuna haja ya kufanya sisi tusonge, kilimo cha mkonge kipae juu Zaidi kwa maslahi ya nchi kiuchumi serikali imetusukuma kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu kama ambavyo tumepewa.

"Kwa hiyo yako mengi ya kumshukuru Dk. Samia kwa yale ambayo amefanya kutusukuma kwa kutekeleza yale malengo ya serikali ambayo tumepewa ya kufikisha tani 230,000 mwaka 2025/26."

Aidha, alisema Waziri Mkuu Mh. Kassim Majaliwa alifanya harakati kubwa za kuhamasisha na kuelezea wananchi namna ambavyo serikali inaiunga mkono bodi na kuhakikisha bodi inafikia malengo ya uzalishaji ya tani 120,000 mwaka 2025.

Kwa mujibu wa ilani ya chama tunapaswa kuwa tumezalisha tani 80,000 ifikapo 2025 sasa wakati maeleekzo haya yanatolewa uzalishaji ulikuwa tani 36,000 kwa mwaka

"Kwa sasa tunazalisha tani 60,000 tumeongeza takribani tani 24,000 lakini yote hii kwa sababu ya mipango mizuri na utayari wa Awamu ya sita kuwezesha bodi kuhakikisha kuwa tunafikia malengo ambayo tumepewa" alisema.




# WAZIRI BASHE AZINDUA KITUO ATAMIZI MKONGE

*Naagiza tupate vifaa vyote muhimu ambavyo vinahitajika kwa ajili ya kufanya shughuli ndogo ndogo za uzalishaji mkonge ili vikundi vya wajasiriamali kina mama na vijana wakipata mkopo wa asilimia 10 wa halmashauri, wana uwezo wa kwenda kununua singa za Mkonge au malighafi hawahitaji kununua mashine, watazikuta hapa.*



Waziri wa Kilimo, Mh. Hussein Bashe ameiagiza Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), kuweka utaratibu mzuri kuhakikisha kunakuwa na vifaa vyote muhimu katika Kituo Atamizi cha Mkonge BBT kilichopo Tanga.

Waziri Bashe amezindua kituo hicho Oktoba mwaka huu ambapo kimelenga kutoa mafunzo ya ubunifu na uzalishaji wa bidhaa za mkono (handcraft) zitokanazo na singa za Mkonge, uzalishaji nzi chuma, utengenezaji wa karatasi, mafunzo ya ukataji na uchakataji Mkonge.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mhe. Bashe alisema kituo hicho kinahitaji kuwa na vifaa ili kina mama, wenye ulemavu na vijana wanaozalisha bidhaa mbalimbali wakija wakute vifaa vyote muhimu ambapo pia watatumia kituo hicho kama sehemu ya kuzalishia mali kisha kwenda kufanya biashara zao nje.

"Naagiza tupate vifaa vyote muhimu ambavyo vinahitajika kwa ajili ya kufanya shughuli ndogo ndogo za uzalishaji mkonge ili vikundi vya wajasiriamali kina mama na vijana wakipata mkopo wa asilimia 10 wa halmashauri, wana uwezo wa kwenda kununua singa za Mkonge au malighafi hawahitaji kununua mashine, watazikuta hapa.

"Mkonge ni zao muhimu sana katika uchumi wa nchi, zipo bidhaa nyingi zinazotokana na mkonge. Bodi imeingia makubaliano na wenzetu ambao wamekuwa wakifundisha namna ya kutumia mabaki ya Mkonge katika kuzalisha karatasi," alisema Mhe. Bashe.

Mh. Bashe alisema Serikali imeweka dhamira kupitia maombi ya bodi takribani Sh milioni 600 kwa ajili ya kuweka Kituo Atamizi Tanga na Zanzibar ambapo Tanga itakuwa kituo ambacho vitawekwa vifaa vyote vidogo vidogo vya kuongeza thamani Mkonge na mazao mengine madogo madogo ya kilimo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mkonge wa TSB, Olivo Mtung'e amesema Kituo hicho kimeanzishwa Tanga kwa sababu Mkonge unalimwa zaidi na ndiyo Makao Makuu ya TSB.

Amesema Kituo hicho Atamizi lengo lake kwanza ni kuwawezesha vijana, wanawake na wenye ulemavu kwa ajili ya kujiajiri lakini pia watakwenda kuwasaidia ambao wanazalisha Mkonge hasa kwa upande wa Tanga ambao walikuwa wanakosa soko la kuuza Mkonge nje.

"Soko letu bado linategemea zaidi kuuza nje huku ndani matumizi siyo makubwa sana lakini tunatambua kuwa vijana wetu, kina mama hawana ajira za kuwaingizia kipato kwa hiyo tunategemea kituo hiki kuwa na watu ambao watajiajiri. Pia tutaongeza matumizi ya zao la Mkonge kwa upande wa ndani.

"Lakini pia kituo hiki ni sehemu ya kwanza tu kuna vituo vingi vinakuja kutakuwa na mashine ya kutengeneza bidhaa za mkono za kufuma kama vile Kamba na cha pili kinaratajiwa kuanzishwa hapa hapa Tanga kwa ajili ya kutengeneza karatasi na gypsum na vitu vya kuezekea," amesema Olivo.



# TSB KUSHIRIKIANA NA ZANZIBAR KUKUZA UTALII, UCHUMI WA BULUU KUPITIA MKONGE

Serikali Visiwani Zanzibar, imefungua milango kwa zao la Mkonge kuanza rasmi katika Soko la Utalii kwa kuhusisha vikundi mbalimbali vya wanawake na vijana wajasiriamali hatua itakayosaidia kukua kwa sekta hiyo na kusaidia wananchi kuwa na uhakika wa kujiongezea vipato.

Katibu Mkuu wa Wizara ya na Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar (WUBU) Dk. Aboud Jumbe amebainisha hayo wakati akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), mjini Unguja ambaye yuko ziarani visiwani humo kwa ajili ya kuhamasisha matumizi ya Mkonge katika mnyororo wa thamani kwa vijana wa Chuo cha Mafunzo na vikundi vya wajasiriamali.

Amesema hatua hiyo iwe ni mwelekeo wa kuanzisha ushirikiano katika sekta ya Uchumi wa Buluu ikiwamo kuangalia uwezekano wa kutumia Mkonge kama sehemu maalumu ambayo inaweza ikasaidia pia sekta za utalii, kilimo na ujenzi wa vitu mbalimbali kama vile boti.

"Wizara yetu imekuwa na sera ya kuwa na milango wazi kwa wadau wote ndani na nje ya nchi kuja katika uwekezaji wa Uchumi wa Buluu. Tuko tayari kushirikiana na bodi hasa katika matumizi ya zao la Mkonge katika maeneo mbalimbali ya Uchumi wa Buluu.

"Nadhani ni jambo jema kuanza kufikiria suala la kuwa na mfumo rasmi kupitia maandiko pamoja na makubaliano ya ushirikiano (MoU), lakini ni jambo jema sana kuanza kufikiria kuja na kongamano kama sehemu ya jukwaa la kutoa elimu ya faida ya zao la Mkonge katika sekta mbalimbali ikiwamo sekta zote za Uchumi wa Buluu.

"Nimefurahishwa na namna ambavyo mmeliingiza suala hili katika soko la utalii hususani katika matumizi ya bidhaa za mkono (handcraft) kwa sababu zao la Mkonge limo katika uvuvi mambo mbalimbali ya ujasiriamali na kilimo na wananchi hao hao ndiyo huzungusha katika kilimo cha zao la mwani, kwa hiyo zao la mkonge lina fursa ya kuzunguka katika ule mnyororo wa thamani wa kaya na sekta mbalimbali na kumarisha hali ya maendeleo ya sekta ya buluu.

"Tuko tayari kuingia katika utekelezaji wa masuala mbalimbali ikiwa ni utekelezaji wa ikiwa ni utafiti, teknolojia, elimu, uelewa lakini pia kusaidia kutupa zile mbinu mbalimbali za ubunifu wa zao la Mkonge na masoko kwa wananchi wetu," amesema Dk. Jumbe.

Kwa upande wake Mkurugenzi Kambona ameishukuru WUBU kwa kurahisisha mchakato huo ambapo ameahidi kuvipatia singa za Mkonge vikundi hivyo vya wanawake na vijana wajasiriamali visiwani humo ambazo zitawasaidia kutengeneza bidhaa mbalimbali na kuziuza.

"Sisi tumesema Mkonge ni zao ambalo tunadhani katika Uchumi wa Buluu tungeweza kutumia fursa zilizopo kwa upande Zanzibar kukuza zao la Mkonge kwa upande wa bara kwa kutumia mlango wa utalii.

"Kama ambavyo tumeona wenzetu Wazanzibar sehemu nyingi zikiwamo vikundi na Chuo cha Mafunzo kuna utaalamu wa kutumia singa kutengeneza bidhaa ambapo wanatumia Makumbi ya nazi kutengeneza bidhaa kama vitanda, mapambo...

"Lakini tumeona kuna changamoto katika upatikanaji wa hizo singa lakini inachukua muda mrefu lakini pia hatua zake ni pia zinachukua muda mrefu kidogo.

"Kwa kuwa tuliona tayari utaalamu wa kutengeneza hizo bidhaa tayari upo tunaweza tukatambulisha nyuzi asilia nyingine ambayo ni ya zao la Mkonge wanaweza kuendelea nayo mbele lakini si kwa ajili ya kuiondoa ile ya utengenezaji wa kutumia usumba lakini wanaweza kutumia mkonge wakati wanasubiri Makumbi ya nazi kuwa tayari," amesema Kambona.

Aidha, Pamoja na mambo mengine amesema TSB itaanza kuwasambazia nyuzi za mkonge kwa muda fulani lakini baadaye wakiweza kujisimamia watakuwa wanafanya biashara.

*"Kwa kuwa tuliona tayari utaalamu wa kutengeneza hizo bidhaa tayari upo tunaweza tukatambulisha nyuzi asilia nyingine ambayo ni ya zao la Mkonge wanaweza kuendelea nayo mbele lakini si kwa ajili ya kuiondoa ile ya utengenezaji wa kutumia usumba lakini wanaweza kutumia mkonge wakati wanasubiri Makumbi ya nazi kuwa tayari," amesema Kambona.*

# MAAGIZO MANNE YA MHE. BASHE KWA BODI YA WAKURUGENZI TSB

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussien Bashe ametoa maagizo manne kwa Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), yenye wajumbe tisa baada ya kuizindua mapema mwaka huu.

Bodi hiyo ambayo Mwenyekiti wake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi imezinduliwa baada ya bodi zamani kumaliza muda wake wa miaka mitatu kwa mujibu wa sheria.

Katika maagizo yake Mhe. Bashe ameitaka bodi kuifanya menejimenti kuwa mwezeshaji badala ya mdhibiti, kupitia upya mfumo wa masoko nje ya nchi, miundombinu rafiki na kuhakikisha uzalishaji unaongezeka.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo iliyofanyika jijini Dodoma, Mhe. Bashe ameitaka bodi hiyo kuifanya menejimenti kubadilika kutoka kuwa Mdhibiti pekee na Mwezeshaji sanjari na kuandaa miundombinu rafiki itakayofanikisha kuongeza tija kwa zao hilo.

Aidha, ameitaka bodi hiyo mpya kupitia upya mfumo wa masoko wa kuuza mkonge ili kuhakikisha mkulima anapata soko la uhakika na lenye maslahi.

"Nendeni mkatazame mfumo wetu wa kuuza mkonge je, tukauze kwa mnada? Mkatazame ni namna kufanikisha hayo lakini pia bodi haitakiwi ikae Tanga tu tupambane kuhakikisha zao hili linakua, tuongeze uzalishaji na kutafuta masoko kimataifa.

"Licha ya hayo, ni lazima bodi isimamie wadau wake pale inapoona wana matatizo na watu wengine, ni lazima iwe mbele wakati mdau yuko nyuma na tuondokane na dhana ya kufikiri kuwasimamia wakulima bila kuwawezesha, utamsimamia sawa je akivuna akitaka kuuza tunanunua sisi?" alisema.

Pamoja na mambo mengine, Mhe. Bashe aliipongeza bodi iliyomaliza muda wake kwa kusimamia maelekezo ya serikali licha ya kupitia changamoto mbalimbali.

"Nawapongeza kwani mmechukua jukumu wakati uzalishaji ulikuwa tani 20,000 na leo tunazungumzia zaidi ya 50,000. Bodi mpya inakuta bodi ina ofisi, mali zilizoko mahakamani zimerudishwa," amesema Mhe. Bashe.

Awali, Mwenyekiti Sabi alisema; "tunafahamu ziko changamoto kadhaa lakini fursa kubwa iliyopo kwenye Sekta ya Mkonge, tunakuahidi kufanya kazi kwa weledi mkubwa kuanzia leo ambapo unazindua bodi hii.

"Tunatoa shukrani za dhati kwa bodi inayomaliza muda wake kwa kuifanya kazi kwa ufasaha hadi leo wanapotukabidhi bodi hii."

Naye Mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Mariam Nkumbi alisema bodi ilifanikisha urejeshwaji wa mali za serikali yakiwamo mashamba na majengo, ukarabati wa jengo la ofisi ya bodi, kuongeza idadi ya watumishi na mengine mengi.




> *Licha ya hayo, ni lazima bodi isimamie wadau wake pale inapoona wana matatizo na watu wengine, ni lazima iwe mbele wakati mdau yuko nyuma na tuondokane na dhana ya kufikiri kuwasimamia wakulima bila kuwawezesha, utamsimamia sawa je akivuna akitaka kuuza tunanunua sisi?" alisema.*

# BANDARI YA TANGA INAVYORAHISISHA USAFIRISHAJI MKONGE




*Kumekuwa fursa na changamoto mbalimbali zinatokana na zao hilo la Mkonge kupitia Bandari yetu ya Tanga lakini baada ya maboresho yaliyofanyika katika bandari hiyo sasa hivi wadau na wazalishaji wote wa zao la Mkonge waje kutumia bandari yetu ya Tanga na zile gharama kubwa ambazo zimekuwa zikisababisha wakimbie Sasa hazipo tena.*





Bandari ya Tanga imekuwa ikihudumia mazao mbalimbali yanayopakiwa na kusafirishwa kupitia Bandari ya Tanga Kwenda jijini Dar es Salaam na nchi mbalimbali ikiwamo Mkonge.

Kwa kipindi cha miezi mitano Julai-Novemba 2024 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Bandari ya Tanga imefanikiwa kusafirisha jumla ya Tani 4,811 za Mkonge.

Meneja wa Bandari ya Tanga, Masoud Mrisha anasema maboresho ya bandari hiyo ambayo kwa sasa yamefikia asilimia 99.6 kadiri siku zinavyokwenda milango ya kibiashara inazidi kufunguka na wafanyabiashara kuonyesha nia ya kuitumia bandari hiyo hatua ambayo itazidi kuchangia kuongezeka kwa pato la taifa.

"Kumekuwa fursa na changamoto mbalimbali zinatokana na zao hilo la Mkonge kupitia Bandari yetu ya Tanga lakini baada ya maboresho yaliyofanyika katika bandari hiyo sasa hivi wadau na wazalishaji wote wa zao la Mkonge waje kutumia bandari yetu ya Tanga na zile gharama kubwa ambazo zimekuwa zikisababisha wakimbie Sasa hazipo tena.

"Katika kipindi cha miaka mitano 2019/20-2023/24 Bandari ya Tanga imefanikiwa kuhudumia jumla ya tani 44,552 za Mkonge na kwa kipindi cha miaka mitano imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 0.6 kwa mwaka," anasema Mrisha.

Anasema kwa ujumla kukamilika kwa mradi huo kumekuwa ni chachu ya maendeleo na ufunguo kwa ushoroba wa Kaskazini ambapo Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) itaendelea kusimamia vema na kuutunza ili uweze kuzalisha na kuirudishia serikali faida kabla ya muda wa marejesho ya gharama zilizowekezwa.

"Aidha, nawasihi serikali na wadau wengine kama sekta binafsi waendelee kutekeleza mipango ya kuboresha miundombinu ya usafirishaji wa nchi kavu hasa reli na kuwekeza katika kilimo cha biashara na viwanda katika mikoa inayozunguka Bandari ya Tanga ili kuchochea matumizi ya Bandari ya Tanga," anasema.



*Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Saddy Kambona (mwenye suti kulia) akipokea sampuli ya nzi chuma (black soldier flies) na mbolea kutoka kwa Dk. Aziza Konyo Sampuli hizo zimetokana na uongezaji thamani kwa kutumia mabaki ya Zao la Mkonge (sisal waste). Nzi chuma hutumika kama protini muhimu katika vyakula vya mifugo jamii ya ndege, wanyama na binadamu.*

# UTAFITI: MABAKI YA MKONGE HUZALISHA NZI CHUMA, MBOLEA

*"TSB ina mahusiano ya muda mrefu na Chuo cha Nelson Mandela katika kufanya tafiti mbalimbali kuhusu uongezaji thamani wa zao la mkonge. Kwa hiyo Aziza chini profesa wake Anthony Mshandete na Revocatus Machunda amefanya utafiti wa kuzalisha nzi chuma (black soldier flies) kutokana na mabaki ya mkonge (sisal waste) ambayo hutumika kama protini kwenye chakula cha mifugo jamii ya ndege wanyama na binadamu;" amesema Kambona.*



Imezoeleka mkonge baada ya kuchakatwa na kupatikana singa (sisal fibre) mabaki yake (sisal waste) hutupwa kama uchafu kwa kuwa hayana matumizi mengine.

Hatua hiyo ni tofauti kwa Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu (PhD), katika Chuo Kikuu cha Afrika cha Nelson Mandela cha Sayansi na Teknolojia (NM-AIST) kilichopo mkoani Arusha, Aziza Konyo ambaye pia ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), amefanya utafiti na kuzalisha nzi chuma (black soldier flies) na mbolea kwa kuongeza thamani kwa kutumia mabaki hayo ya mkonge.


Akizungumza baada ya kikao cha uwasilishaji wa ugunduzi wa utafiti huo, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Saddy Kambona amesema utafiti huo ambao umesajiliwa kwa hati miliki pia umebaini licha ya kuzalisha protini kutengeneza chakula cha mifugo na mbolea lakini pia mabaki ya chakula wanachokula nzi chuma hao ni mbolea nzuri inayotumika katika mazao mbalimbali.

"Bodi imepokea wasilisho la utafiti huo na imefurahi kuona kwamba zao la mkonge linazidi kupata thamani kwa sababu tumezoea baada ya kupatikana singa basi kinachobaki chote ni uchafu kinatupwa.

"TSB ina mahusiano ya muda mrefu na Chuo cha Nelson Mandela katika kufanya tafiti mbalimbali kuhusu uongezaji thamani wa zao la mkonge. Kwa hiyo Aziza chini profesa wake Anthony Mshandete na Revocatus Machunda amefanya utafiti wa kuzalisha nzi chuma (black soldier flies) kutokana na mabaki ya mkonge (sisal waste) ambayo hutumika kama protini kwenye chakula cha mifugo jamii ya ndege wanyama na binadamu," amesema Kambona.

Utafiti huu ni wa pili kufanyika na chuo hicho ambapo utafiti wa kwanza unatekelezwa na chuo hicho kwa ushirikiano na Serikali ya Denmark kupitia Shirika lake la Maendeleo (Danida), ambapo umejikita katika maeneo matatu ambayo ni uzalishaji gesi asilia, ujenzi na kile kitakachozalishwa kutokana na gesi asilia.













# HISTORIA YA MKONGE KWENYE NEMBO YA BoT

Zao la Mkonge ndiyo zao pekee kuwahi kuchangia kiwango kikubwa cha fedha katika bajeti ya Serikali katika miaka ya 1960-1970 ambapo ilikuwa ikichangia asilimia zaidi ya asilimia 60.

Mkonge pia ndiyo zao pekee katika historia ya kilimo nchini kuiingizia nchi fedha nyingi za kigeni kwa asilimia 65.

Kutokana na hali hiyo, kwa heshima ya zao la Mkonge bajeti hiyo ya serikali ilikuwa inafanyikia mkoani Tanga ambako ndiyo asili ya Mkonge katika Hoteli ya Mkonge (Mkonge Hotel) ambayo hadi leo ipo.

Mkonge pia ulipewa heshima nyingine kubwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kuweka zao la Mkonge kwenye nembo yake ambayo pia imetumika kwenye baadhi ya noti za zamani ikiwamo noti ya Sh 500, 200, 100, 50 nyinginezo.

Pamoja na mambo mengine, mwaka 1966, BoT ilitoa noti za kwanza zenye thamani za Sh tano, 10, 20 na Sh 100 ambapo upande wa mbele wa noti hizo kulikuwa na sura ya Rais wa Kwanza wa Tanzania, hayati Mwalimu Julius Nyerere kwenye baadhi ya matukio ya kupata uhuru na upande wa nyuma ulionyesha mambo mbalimbali yahusuyo Tanzania.

Katika noti hizo, noti ya Sh 10 ilikuwa na shamba la Mkonge na singa za Mkonge (Sisal Fiber) zikiwa zimeanikwa baada ya kuchakatwa.

Noti hizo ziliendelea kutumika hadi mwaka 1978 zilipofanyiwa mabadiliko mengine.

Kwa hiyo yale majani ya dhahabu kwenye Nembo ya BoT ni zao la Mkonge zao ambalo mwaka 2020 Serikali imeliingiza katika mazao ya kimkakati.



# WAZIRI BASHE ABAINISHA MIKAKATI YA SERIKALI KUONGEZA UZALISHAJI ZAO LA MKONGE 2024/25

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe amebainisha mikakati ya serikali katika kuongeza uzalishaji wa zao la Mkonge kutoka tani 56,732.69 mwaka 2023/2024 hadi tani 80,000 mwaka 2024/2025.

Akiwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka 2024/2025, Mhe. Bashe alisema Wizara yake kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB) lengo hilo litafikiwa kwa kununua zana za kilimo kwa ajili ya kuwezesha uendelezaji wa mashamba makubwa ya pamoja na kununua mashine ya kuchakata mkonge(korona).

"Pamoja na mambo mengine, tutaendeleza miundombinu ya kituo cha uchakataji cha Handeni, kukarabati miundombinu ya shamba la Kibaranga na kuwezesha umiliki wa ardhi ya kilimo yenye ukubwa wa hekta 6,000 kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja katika mikoa ya Tanga, Singida na Morogoro.

"Aidha, Bodi itaratibu usambazaji wa miche ya Mkonge milioni tatu katika maeneo ya uzalishaji na kupitia TARI itatoa mafunzo kuhusu uzalishaji wa Mkonge na fursa zitokanazo na zao hilo kwa wadau 100,000 na maafisa ugani 500," alisema Mhe. Bashe.

Mhe. Bashe amesema katika kuongeza matumizi ya mmea wa Mkonge, Bodi kwa kushirikiana na Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela (NM-AIST), itajenga kituo cha uzalishaji wa Inzi chuma (black soldier flies) kwa kutumia mabaki ya Mkonge (Sisal waste) ili kutengeneza protini kwa matumizi ya binadamu na mifugo (wanyama, ndege na samaki).

"Pia, Bodi itawezesha utafiti wa zao la Mkonge utakaofanywa na watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), TARI-Mlingano, Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela (NM-AIST) kwa kushirikiana na Kampuni ya Carbonovia UK ya Oxford Uingereza kuhusu uwezekano wa kuzalisha protini kutokana na hewa ukaa (Carbon dioxide) kutoka kwenye mabaki ya Mkonge.

"Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza na Chuo cha Mafunzo Zanzibar itaanzisha na kuimarisha utaalamu wa uzalishaji wa bidhaa za mikono za Mkonge ili kutengeneza ajira kwa vijana na wanawake," alisema Mhe. Bashe.

> ***Pia, Bodi itawezesha utafiti wa zao la Mkonge utakaofanywa na watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), TARI-Mlingano, Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela (NM-AIST) kwa kushirikiana na Kampuni ya Carbonovia UK ya Oxford Uingereza kuhusu uwezekano wa kuzalisha protini kutokana na hewa ukaa (Carbon dioxide) kutoka kwenye mabaki ya Mkonge.***



# ZIARA YA WAKURUGENZI TSB MKOANI TANGA







Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), ikiongozwa na Mwenyekiti wake Theobald Sabi, wamefanya ziara ya kutembelea miradi mbalimbali ya Mkonge mkoani Tanga ikiwamo mashamba na viwanda vya uchakataji Mkonge.

Lengo la ziara hiyo ni kujionea shughuli husika katika Sekta ya Mkonge na changamoto zinazowakabili wakulima na wote waliopo kwenye mnyororo mzima wa Sekta ndogo ya Mkonge.

Katika ziara hiyo, wajumbe hao wametembelea mashamba ya Hale na Magunga na viwanda vya uchakataji Mkonge.







*Mashine ya kuchakata Mkonge (korona) ikiwa imeshushwa tayari kwa kusimikwa katika eneo la Taula Kituo cha Handeni mkoani Tanga.*

# SERIKALI KUANZISHA VITUO VYA UCHAKATAJI MKONGE



*Kwa hiyo kwa sasa hivi kuna kituo kikubwa kinajengwa eneo la Taula wilayani Handeni ambapo mashine zimeshaanza kufungwa au kusimikwa. Lakini kuna mashine nyingine nne zinakuja kwa ajili ya Wilaya za Mkinga, Lushoto, Kilosa," amesema Mkurugenzi Kambona.*

Serikali imeanzisha vituo vya uchakataji mkonge ili wakulima wadogo kuchakata kwenye vituo vikubwa katika maeneo ya Lushoto, Mkinga Kilosa na maeneo yote ambayo yana wakulima wadogo.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Saddy Kambona amesema lengo la vituo hivyo ni kurahisisha hatua ya uchakataji Mkonge kwa wakulima wadogo ambapo wanaweza kuhudumiwa kwa mara moja kwenye eneo moja.

"Mashine (korona) hizi ni ghali hivyo si rahisi kwa mkulima mmoja mmoja kujiwekea mwenyewe au kuwa na kituo chake cha kuchakata ingawa ziko mashine ndogo ndogo lakini kuna changamoto ya ubora ndiyo maana tumeamua kuwekeza kwenye vituo hivyo.

"Kwa hiyo kwa sasa hivi kuna kituo kikubwa kinajengwa eneo la Taula wilayani Handeni ambapo mashine zimeshaanza kufungwa au kusimikwa. Lakini kuna mashine nyingine nne zinakuja kwa ajili ya Wilaya za Mkinga, Lushoto, Kilosa," amesema Mkurugenzi Kambona.

Pia amezungumzia kuhusu wakulima wadogo kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha ikiwamo benki ambapo amesema kumekuwa na changamoto kubwa wengi wamekuwa wakilalamika kuna ugumu kidogo katika namna ya kupata mikopo kwenye taasisis hizo.

"Kutokana na hali hiyo, tulifanya jitihada za kukutana na watu wa mabenki tukatengeneza mwongozo wa uwezeshaji kifedha wa Sekta ya Mkonge ambayo tutaizindua kwenye mkutano wa wadau unaokuja.

"Kwenye huo mwongozo wajibu wa bodi, benki, mkulima na wadau wengine unaonekana wazi kwa wote ni namna gani anaweza akakopesha au kukopesheka huo mwongozo umerahisisha hivyo," amesema.



# TSB YAGAWA SINGA ZA MKONGE KWA WAJASIRIAMALI ZANZIBAR

*"Bodi ya Mkonge imeangalia rekodi ya uzalishaji wa bidhaa za mkonge tangu mwaka 2020 ambapo tulifanya vizuri kidogo ambapo tulifanikiwa kuingiza takribani Sh biloni saba kutokana na bidhaa za mkonge lakini pia tukauza nje Dola milioni 5.78," alisema Kambona.*

Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), imegawa Singa za Mkonge (Sisal Fiber) tani 9.6 zenye thamani ya Sh milioni 40 kwa kwa ajili ya vikundi vya wajasiriamali wanawake, wenye ulemavu na vijana wa Zanzibar wanaozalisha bidhaa za Mkonge kwa kutumia mikono (handcraft).

Hatua hiyo inatokana na ahadi ya Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB) Saddy Kambona aliyoitoa Februari 22 mwaka huu, Mjini Unguja alipotembelea vikundi mbalimbali vya wanawake na vijana wajasiriamali waliopo Unguja.

Akizungumza katika hafla ya ugawaji wa singa hizo, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud alisema nyuzi hizo zitagawiwa katika vikundi 20 vya wajasiriamali visiwani humo.

Mkuu huyo wa mkoa amewataka wajasiriamali hao kuiona hiyo ni fursa na kuitumia vema kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla kwani wanapozalisha kwa wingi watauza nje ya nchi na hivyo nchi itapata fedha nyingi za kigeni.

"Sisi tutaendelea kuwasemea vema Bodi ya Mkonge niwashukuru Wizara ya Utalii kwa kuunganisha Mkonge na utalii na Wizara ya Uchumi wa Buluu kwa kuunganisha Mkonge na uchumi wa buluu.

"Kwa sababu uchumi wa buluu unakwenda kugusa moja kwa moja kwenye boti kadhalika na wale wanaolima mwani kwani miongoni mwa bidhaa mtakazozalisha ni kamba ambazo zitakwenda kufunga mwani.

"Lakini jambo jingine ambalo litafanyika licha ya kupata elimu na kuzingatia ubora wa bidhaa zenu mtaunganishwa na masoko ya moja kwa moja nje ya nchi na haya ndiyo viongozi wa nchi yetu waliahidi," alisema.

Naye Mkurugenzi Kambona alisema Bodi ya Mkonge inao wajibu wa kuhakikisha inaongeza matumizi ya mkonge ndani ya nchi na hilo linafanikiwa kwa kuwafanya wananchi wapende bidhaa zinazotokana na zao hilo na zinazozalishwa nchini.

"Moja ya mkakati wa bodi ni kuhakikisha tunarudisha uzalishaji wa bidhaa kwa kutumia mikono na mashine nyepesi kwa wananchi wetu na eneo moja ambalo tumeliona ni Zanzibar ndiyo maana tunazindua huu mradi hapa na bara tutazindua mwezi ujao.

"Bodi ya Mkonge imeangalia rekodi ya uzalishaji wa bidhaa za mkonge tangu mwaka 2020 ambapo tulifanya vizuri kidogo ambapo tulifanikiwa kuingiza takribani Sh biloni saba kutokana na bidhaa za mkonge lakini pia tukauza nje Dola milioni 5.78," alisema Kambona.

Aidha, alisema wajasiriamali hao waliopatiwa singa za mkonge watapatiwa mafunzo ya namna bora ya kuzalisha bidhaa hizo kwa kutumia mashine nyepesi.



# TSB NA MKAKATI WA KUHAMASISHA MATUMIZI YA BIDHAA ZA MKONGE NCHINI

Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), imejipanga kuhakikisha inaongeza matumizi ya mkonge bidhaa zitokanazo na mkonge kwa kuhamasisha Watanzania kupenda bidhaa hizo.

Lengo la hatua hiyo ni kuongeza uzalishaji mkonge na matumizi ya bidhaa zinazotokana na mkonge.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Saddy Kambona amesema katika kuhamasisha matumizi ya ndani ya mkonge maana yake ni kwamba wanahamasisha watu kwanza kupenda bidhaa za mkonge na kuhamasisha wanawake na vijana kujiunga na vikundi mbalimbali ili wapatiwe mafunzo ya namna ya kuzalisha hizi bidhaa za mikono (handcraft).

"Tunategemea bidhaa nyingi zikizalishwa na matumizi pia yataongezeka. Yako mambo mengi ambayo tumefanya kujaribu kutatua hizi changamoto ambazo wakulima wetu wamekuwa wakizipitia na kwa mujibu wa mpango mkakati wa kukuza sekta maeneo mengine ambayo tunafanya kama wajibu wetu Bodi ya Mkonge ni kuhakikisha tunaongeza matumizi ya mkonge ndani ya nchi," alisema.

Alisema kwa sasa asilimia 70 ya mkonge wote unaozalishwa nchini unapelekwa nje ambapo kuna nchi zaidi ya 26 zinanunua mkonge hapa nchini na mkakati ambao Bodi inafanya ni kurudisha biashara ya mkonge duniani

Aidha, alisema China ndiyo mnunuzi mkubwa wa mkonge kutoka Tanzania ambapo asilimia 50 ya mkonge wote unakwenda China lakini ziko nchi za Afrika kama Nigeria, Ghana, Guinea, Tunisia, Misri, Afrika Kusini, Kenya wote wananunua mkonge kutoka Tanzania

"Baada ya soko la Ulaya kuyumba na kutetereka sana hii hatua ya kugundua masoko mapya katika nchi za Afrika imefanya sekta ya Mkonge kuchangamka sana," alisema.

> ***Tunategemea bidhaa nyingi zikizalishwa na matumizi pia yataongezeka. Yako mambo mengi ambayo tumefanya kujaribu kutatua hizi changamoto ambazo wakulima wetu wamekuwa wakizipitia na kwa mujibu wa mpango mkakati wa kukuza sekta maeneo mengine ambayo tunafanya kama wajibu wetu Bodi ya Mkonge ni kuhakikisha tunaongeza matumizi ya mkonge ndani ya nchi," alisema.***



# SERIKALI AWAMU YA SITA ILIYOJIKITA KUINUA SEKTA YA MKONGE



Tangu kuapishwa kwake kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amejitahidi kuongoza kwa kugusia na kusimamia ipasavyo sekta mbalimbali ikiwamo moja ya sekta nyeti ya kilimo.

Katika siku zake 100 madarakani, Rais Samia alifuta mashamba 11 yenye ukubwa wa ekari 24,161 mkoani Morogoro katika Wilaya za Kilosa na Mvomero ambapo yamegawiwa kwa wakulima wakiwamo wa Mkonge ambalo ni moja ya mazao ya kipaumbele yanayotakiwa kulimwa katika mashamba hayo.

Mashamba yenye jumla ya ekari 8,000 kati 24,000 yalishagawiwa kwa wakulima wadogo wa Mkonge na wananchi kwa mfumo wa Block Farming ili kuongeza ufanisi zaidi lakini pia wakulima watapewa elimu ya kuunda Vyama vya Ushirika (AMCOS) ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wake unaendelea.

Katika mashamba hayo, mazao ya kipaumbele yaliyopendekezwa ni Mkonge na miwa kulingana na maeneo husika ambapo pia wananchi wataruhusiwa kilimo mseto kwa kuchanganya Mkonge na mazao mengine ya chakula ya muda mfupi.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Saddy Kambona anamshukuru Rais Samia kwa kufuta hati za mashamba pori hayo na kuelekeza kuwa baadhi ya mashamba hayo yawe chini ya Bodi ya Mkonge ili yagawiwe kwa wakulima na kuongeza kuwa hatua hiyo ni muhimu kwa sekta ya Mkonge nchini.

"Bodi inapenda kutoa shukrani nyingi na za pekee kwa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kwa hatua za makusudi alizochukua za kufuta mashamba pori katika Wilaya za Kilosa na Mvomero mkoani Morogoro na kuelekeza kuwa baadhi ya mashamba hayo yakabidhiwe kwa Bodi ya Mkonge Tanzania ili Bodi igawe kwa wakulima wadogo kwa ajili ya kilimo cha Mkonge.

"Hatua hii ya Mheshimiwa Rais, imeiwezesha Bodi kupata ardhi takriban Ekari 25,000 ambazo zimegawiwa kwa wakulima wadogo kwa ajili ya kilimo cha Mkonge ambapo jumla ya takribani Ekari 8,000 zimegawiwa kwenye mashamba ya Mbugani Sisal Estate, Manyenyere Sisal Estate, Magole Sisal Estate, Chanzuru Sisal Estate, Msowero Sisal Estate na mengineyo," anasema Mkurugenzi Kambona.

Kambona anasema katika mashamba hayo kipaumbele ni wanawake, vijana na wenye ulemavu ambapo hadi sasa zaidi ya Ekari 8,000 zimegawanywa kwa wakulima wadogo ili kulima Mkonge na kati ya hizo takribani Ekari 3,000 zimegawanywa kwa makundi ya vijana.

"Inakadiriwa kuwa takribani vijana 6,000 wanajishughulisha na kilimo cha Mkonge nchi nzima. Elimu bado inaendelea kutolewa kwa wananchi hasa vijana ili kujiunga kwenye kilimo cha Mkonge," anasema Mkurugenzi Kambona.

Kwa mujibu wa taarifa ya Timu ya Usimamizi wa Ugawaji mashamba ikishirikiana na Bodi ya Mkonge, ilifanya kazi ya kuwaelimisha viongozi wa vijiji na wananchi juu ya uundaji wa vikundi vya ushirika vya wakulima (Amcos) na kutoa maelekezo ya serikali kuhusu vigezo na vipaumbele katika ugawaji wa mashamba hayo.

Katika maelekezo hayo imeelekezwa kuwa mazao ya kipaumbele ni Mkonge na miwa huku wananchi wote wanaoomba mashamba kupitia taratibu zilizoelekezwa kuanzia ngazi ya kitongoji, mkutano mkuu wa kijiji na Baraza la Maendeleo la Kata wakipata fursa ya kupatiwa mashamba.

**Historia ya mashamba hayo**

Kwa muda mrefu idadi kubwa ya mashamba hayo yamekuwa yakimilikiwa na wawekezaji pamoja na watu wengine ambao si wanavijiji. Hali hiyo ilisababisha migogoro ya ardhi ya mara kwa mara kwa wanavijiji watumiaji wa ardhi hiyo kutokana na kupambania ardhi kwa matumizi ya kilimo na ufugaji.

Mwaka 2021 Rais Samia alifanya uamuzi wa kubatilisha na kufuta hati za umiliki wa baadhi ya mashamba ya wawekezaji ambayo hayakuendelezwa kwa muda mrefu.

Lengo la kubatilisha umiliki wa mashamba hayo ni kuyarudisha kwa wakulima na wafugaji kwenye wilaya husika ambao ndiyo waliokuwa wakilalamika kwa miaka mingi wakitaka kupatiwa ardhi ya kilimo na ufugaji.

**Ajira kwa wanawake na wanaume**

Ndani ya miaka miwili tu akiwa madarakani kumekuwa na ongezeko la asilimia nne ya ajira kwa wanawake zilizotokana na Zao la Mkonge ambapo Mwaka 2021 Wanawake 110,745 sawa na asilimia 36 walitokana na ajira zilizotengenezwa na sekta nzima ya Mkonge.

Mwaka 2022 Wanawake 190,121 sawa na asilimia 40 ya ajira zilizozalishwa na sekta ya Mkonge.

Wanaume katika Sekta nzima ya Mkonge katika miaka miwili walipungua kwa asilimi sita ambapo mwaka 2021 walikuwa 196,881 sawa na asilimia 64 na mwaka 2022 walikuwa 285,181 sawa na asilimia 60.

# UZALISHAJI MKONGE WAONGEZEKA, WAFIKIA TANI 59,000

- NI ONGEZEKO LA TANI 10,000 KUTOKA MWAKA 2022/23 SAWA NA 19%

Katika kipindi cha Mwaka 2022/23 uzalishaji mkonge umeongezeka kutoka tani 49,752.88 hadi kufikia tani 59,416.28 mwaka 2023/24 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 19%.

Aidha, mauzo ya singa za mkonge nje ya nchi yameongezeka kutoka tani 31,572.42 mwaka 2022/2023 hadi kufikia tani 33,535.26 mwaka 2023/2024.

Kutokana na mauzo hayo, mapato ya mauzo ya singa nje ya nchi yameongezeka kutoka Dola za Marekani 54,556,093.81 mwaka 2022/2023 hadi kufikia Dola za Marekani 54,816,095.71 mwaka 2023/2024 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 6.22%.

**Bidhaa za Mkonge**

Uzalishaji wa bidhaa za Mkonge umeongezeka hadi kufikia tani 2440.99 mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na tani 1965.11 za mwaka 2022/2023 ikiwa ni ongezeko la asilimia 24%.

Mauzo ya bidhaa za mkonge kwa mwaka 2022/2023 yalikuwa tani 1176.21 yenye thamani ya Dola za Marekani 2,624,204.52 huku mauzo ya bidhaa hizo kwa mwaka 2023/2024 yakiwa tani 1867.52 yenye thamani ya Dola za Marekani 4,105,561.22 ikiwa ni sawa na ongezeko la tani 691.15 sawa na asilimia 58%.

Kwenye eneo la upandaji wa Mkonge kwa mwaka 2022/2023 zilipandwa hekta 7275.16 na mwaka 2023/2024 zimepandwa hekta 9019.35 ikiwa ni ongezeko la hekta 1744.19 sawa na asilimia 24%.



FURSA MKONGENI...

# SABABU TANO KWA NINI WATU WALIME ZAO LA MKONGE



1. Zao lenye uhakika wa soko.
2. Linastahimili ukame.
3. Zao ambalo linapandwa na kuvunwa wakati wowote(halina msimu).
4. Halishambuliwi kirahisi na magonjwa na wadudu waharibifu.
5. Linaweza kuhifadhiwa kwa kipindi kirefu bila kupoteza ubora wake kwa kiwango kikubwa.

**FURSA ZILIZOPO KWENYE ZAO LA MKONGE**

Zao la Mkonge lina fursa nyingi ambapo wakulima wengi hujishughulisha nacho kama njia ya kuimarisha uchumi wao. Mkonge ni zao linaloweza kuleta faida kubwa kutokana na mahitaji yake makubwa katika soko la kimataifa, hasa katika uzalishaji wa bidhaa za nyuzi kama vile, mazuria, mabegi, vikapu, vijaa vya ujenzi nk.

Unapofanya kilimo/biashara ya mkonge tegemea kufaidika na fursa zilizopo kwenye zao hilo kama vile;

1. Kufanya biashara ya singa(sisal fiber)ndani na nje ya nchi.
2. Kuanzisha viwanda vya kusindika majani ya mkonge(korona).
3. Kuanzisha viwanda vya kutengeneza bidhaa za mkonge kama vile gypsum.
4. Kuanzisha viwanda vya kukamua asali ya mkonge(sisal inulin).
5. Kuanzisha kampuni za kutoa huduma ya uandaaji wa mashamba ya mkonge.
6. Kutengeneza mtambo ya uchakataji mkonge kama vile korona, kayamba na press inayotumika kubana marobota ya mkonge.
7. Kuzalisha chakula cha wanyama kwa kutumia mabaki ya mkonge.
8. Kuzalisha nishati(biogas)kwa kutumia mabaki ya mkonge.



# WANAFUNZI ST. MARGARETS ACADEMY WAFUNDWA KILIMO CHA MKONGE, FAIDA ZAKE

Wanafunzi wa Shule ya Msingi St. Margarets Academy iliyopo mkoani Arusha, wamefanya ziara ya mafunzo Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB) kwa lengo la kujifunza kuhusu kilimo cha Mkonge na faida zake.

Ziara hiyo iliyofanyika Novemba mwaka huu, inawafikisha wanafunzi hao katika Kituo cha Utafiti cha Utafiti wa Udongo na Zao la Mkonge (TARI Mlingano), ambako wamejifunza historia ya zao la mkonge, mbinu za kilimo chake, na utafiti unaofanyika katika utengenezaji wa mbegu za Mkonge kwa njia ya maabara (Tissue Culture).

Aidha, wametembelea Kiwanda kinachozalisha bidhaa za Mkonge cha Sisalana ambako walijionea michakato ya utengenezaji na bidhaa zinazotokana na zao hilo.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Dorice Lukumai, aliushukuru uongozi wa TSB kwa kuwakaribisha na kutoa mafunzo kwa wanafunzi.

"Wanafunzi wetu wamefurahi sana kujifunza mambo mengi kuhusu Mkonge. Tutakaporudi Arusha nina imani tutakuwa mabalozi wazuri wa zao hili," amesema.

Naye mwanafunzi Sabiri Mkama, kwa niaba ya wenzake, alieleza furaha yake kuhusu ziara hiyo; "Leo ni siku njema sana, tumefurahi kuja hapa Tanga na kujifunza mambo mengi kuhusu Mkonge. Mimi nitaendelea kuwafundisha watu wengine faida za Mkonge pamoja na asili yake," amesema Sabiri.





# MAMBO 10 MUHIMU KUHUSU MKONGE


Kulinganisha na mazao mengine ya biashara, kilimo cha Mkonge kina faida nyingi ambazo wengi hawazifahamu, hapa tumekuwekea mambo 10 muhimu ya manufaa ya kilimo cha zao hilo ambalo limewahi kuchangia asilimia 60 ya bajeti ya Serikali.

- ☛Mkonge huvumilia hali mbaya ya hewa ikiwa ni pamoja na ukame, joto kali, mvua nyingi nk.
- ☛Hauhitaji pembejeo nyingi, hivyo unaweza kuzalishwa kwa gharama ndogo.
- ☛Magonjwa ya Mkonge yapo kwa kiasi kidogo ambayo hayawezi kuua kabisa mmea endapo kanuni bora za kilimo cha Mkonge zitafuatwa. Magonjwa yanayoshambulia Mkonge ni zebra, kuoza kwa shina (bole rot) na mabaka kwenye majani (KLS). Na mdudu anayeshambulia zao la Mkonge ni Sisal weevil (tembo wa Mkonge) ambaye pia hana madhara makubwa na kumdhibiti ni rahisi.
- ☛Mkonge huvumilia hali mbaya ya utunzaji. Kwa mfano hata bila kupalilia kabisa (ingawa haishauriwi hivyo) Mkonge hauwezi kufa kwa asilimia 100.
- ☛Ni zao linaloweza kuchanganywa na mazao mengine kama vile mahindi, mazao ya jamii ya kunde nk.
- ☛Mkonge unaweza usivunwe kwa wakati unapokomaa bila kuathiri uzalishaji wake kwa kiasi kikubwa.
- ☛Tofauti na mazao mengine ambayo ubora wake hupungua kadri muda unavyoongezeka yakiwa ghalani, nyuzi za Mkonge zinaweza kuhifadhiwa ghalani kwa muda mrefu bila kuathiri ubora wake ilimradi tu zisipate unyevunyevu. Pia hauliwi na wadudu ikiwa utahifadhiwa sehemu kavu na kwa kuzingatia utunzaji wake kwa kuweka mbao chini kabla ya kuweka robota za Mkonge.
- ☛ Zao la Mkonge halina msimu. Kilimo cha Mkonge kinaweza kufanyika baada ya msimu wa kilimo cha mazao mengine ya biashara na ya chakula au wakati wowote wa mwaka.

  Kilimo cha Mkonge hakihitaji mtaalamu wa hali ya juu, hivyo mkulima ataweza kukifanya mwenyewe kwa msaada kidogo wa Bwana Shamba.
- ☛Baadhi ya bidhaa zake zinaweza kutengenezwa kwa mikono popote hata huko huko vijijini mashamba yalipo kama vile Kamba, vikapu, mikoba, mazuria, virago nk. Na hivyo kuongeza wigo wa ajira na pato hasa kwa wanawake na vijana.

---

# ‘MKONGE HAUTEGEMEI MSIMU’




Mkonge umetajwa kuwa ni zao ambalo soko lake halitegemei msimu kulinganisha na mazao mengine ambapo mkulima au mfanyabiashara anaweza kuvuna na kuuza wakati wowote katika mwaka.

Afisa kilimo wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Emmanuel Lutego alisema kutokana na hali hiyo, wadau wanaotaka kuingia kwenye sekta ya Mkonge hawatakiwi kuhofia masoko kwamba watauza wapi au wakati gani kwani moja ya jukumu la Bodi ya Mkonge ni kuwaunganisha wakulima na masoko ya mkonge.

Pamoja na mambo mengine amesema; “kama nchi tuna mkakati wa kufikisha tani 120,000 ifikapo 2025 kwa hiyo tunahitaji wakulima zaidi na mashine za uchakataji ili kufikia malengo hayo.”

Aidha, ametaja mikakati ya kufanikisha malengo hayo ni kuongeza ukubwa wa mashamba na idadi ya wakulima wa mkonge kwa kuhamisisha na kutoa elimu ya kilimo bora cha mkonge katika mikoa yote inayofaa kwa kilimo cha mkonge.

“Lakini pia tumejipanga kuongeza tija ya uzalishaji, kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za mkonge, kuanzisha vituo vya uchakataji wa mkonge (decortication centres) kwa wakulima wadogo,” alisema Lutego.

# WADAU WA MKONGE, COTECNA WAJADILI USAFIRISHAJI MKONGE NCHINI NIGERIA



Wadau wa Mkonge na Kampuni inayotoa huduma ya ukaguzi na udhibiti wa bidhaa zinazosafirishwa nchini Nigeria (Cotecna), wamekutana na kujadiliana masuala mbalimbali ikiwamo usafirishaji Mkonge nchini humo.

Akifungua semina hiyo iliyofanyika jijini Tanga leo Ijumaa Oktoba 25, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB) Saddy Kambona amesema; "Semina hii ni kwa ajili ya kuelimishana na kuelezana kwa undani umuhimu wa zoezi la ukaguzi wa Mkonge unaokwenda nchini Nigeria na kusikiliza maoni yenu wadau katika kuboresha usafirishaji wa Mkonge nje ya nchi."

Naye Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Cotecna kanda ya Afrika Mashariki Welsey Aondo, amewashukuru wadau wa Mkonge kwa ushiriki wao katika semina hiyo na kwamba maoni waliyotoa yatafanyiwa kazi ili wafanyabiashara hao waweze kunufaika na na usafirishaji wa Mkonge.

"Tumefurahi kuwa hapa na kwa kipekee tunashukuru uongozi mzima wa TSB kwa kutupokea na kujadiliana na wadau wa Mkonge kuhusu mambo yanayohusu Sekta ya Mkonge hususani Programu SONCAP ambayo ni maalumu kwa ajili ya kuhakikisha kuwa bidhaa zinazotoka nje ya Nigeria zinakidhi viwango vya ubora vilivyowekwa na Shirika la Viwango la Nigeria," amesema.

Pamoja na mambo mengine, washiriki wa semina hiyo walionesha nia ya kuendelea kushirikiana ili kuboresha Sekta ya Mkonge huku wakiomba uongozi wa Kampuni ya Cotecna kupunguza gharama za upatikanaji wa cheti cha ubora na usafirishaji wa Mkonge nchini Nigeria.



"*Tumefurahi kuwa hapa na kwa kipekee tunashukuru uongozi mzima wa TSB kwa kutupokea na kujadiliana na wadau wa Mkonge kuhusu mambo yanayohusu Sekta ya Mkonge hususani Programu SONCAP ambayo ni maalumu kwa ajili ya kuhakikisha kuwa bidhaa zinazotoka nje ya Nigeria zinakidhi viwango vya ubora vilivyowekwa na Shirika la Viwango la Nigeria," amesema.*




*Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Suleiman Jaffo (kushoto) akipokea zawadi ya picha ya Mkonge Kaimu Meneja wa Bandari ya Tanga, Peter Millanzi (kulia) wakati alipotembelea kujionea maboresho katika bandari hiyo.*
*Picha hiyo ambayo inaonesha gari ya kubebea mizigo bandarini hapo ikipanga singa za Mkonge kuingiza kwenye kontena tayari kwa kusafirishwa, imeandikwa; "Bandari ya Tanga katika kuhudumia Mkonge."*
*Mkonge ni moja ya bidhaa kubwa zinazosafirishwa kupitia bandari hiyo kwenda sehemu mbalimbali.*

